JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

**Shule ya Sekondari ya Ufundi Mwadui,**
**S.L.P 32,**
**Mwadui – Shinyanga.**

**Barua pepe: mwaduitechnical@gmail.com**
**H/M 0766 069 597 / 0624 294 680 whatsapp**
Kumb.Na. MTSS/FIJ/2024

**18/11/2025**

**KWA ………………………………………..**
**………………………………………..**
**………………………………………..**

---

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS) KIDATO CHA KWANZA 2026 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWADUI UFUNDI.**

1.0 Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na Shule hii katika kidato cha kwanza, 2026, **KARIBU SANA MWADUI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**. Shule hii ni ya mchepuo wa Ufundi na ni mchanganyiko( Wavulana na wasichana). Nina imani kubwa kwamba utafurahia kusoma katika shule hii.

Shule ya Sekondari ya Ufundi Mwadui ipo Mkoa wa Shinyanga Wilaya ya Kishapu,ndani ya Mgodi wa Almasi Mwadui ¼ km kutoka Geti la kuingilia Mgodini na ipo umbali wa kilometa 3 kutoka Barabara kuu ya Shinyanga –Mwanza. Ukisafiri kwa Mabasi ya kutoka mikoani,unaelekezwa kuteremka katika stendi ya mabasi ya Maganzo ambapo utachukua usafiri wa Bajaji/Pikipiki hadi Shuleni kwa nauli isiyozidi Tshs 2,000/=

**2.0 SARE ZA SHULE.**

**WASICHANA**

- Sketi mbili rangi ya samawati (dark blue), kwa wasichana wa kiislamuni Hijabu
- Blauzi/shati nyeupe mikono mifupi Jozi mbili (02).
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba,siyo buti na visigino virefu.
- Soksi nyeupe.
- Sweta rangi ya blue ambalo mzazi atalinunua hukohuko.
- Tshirt kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa ambazo zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 12,000/=

**Sketi zinatakiwa kushonwa katika mtindo wa Rinda box, ziwe ndefu kukaribia kugusa viatu.Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa sketi fupi,zinazobana,zisizo na marinda na zenye mpasuo. Nguo ya Kushindia ( Shamba dress ) itakuwa Sketi rangi Nyeusi ambayo atakuja nayo**

**WAVULANA**

- Suruali rangi ya samawati (dark blue) Jozi mbili (02)
- Shati nyeupe mikono mifupi Jozi mbili (02)
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba,siyo buti na visiwe na visigino virefu.
- Soksi rangi nyeusi.
- Mkanda mweusi ngozi wenye kifungio cha kawaida
- Sweta rangi ya blue ambalo mzazi atalinunua hukohuko.
- Tshirt kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa ambazo zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 12,000/=

**Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa suruali zinazobana (Vimodo), Suruali chini ziwe na upana wa inchi 17 au 18, mbele iwe na rinda mbili ("celebration") kila upande na mifuko miwili ya "cross" na nyuma iwe na mmoja. Aidha, inatakiwa iwe na luksi sita za kuweka mkanda. Nguo ya kushindia itakuwa Suruali Nyeusi ambayo Mwanafunzi atakuja nayo**

**3.0 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI.**

Mzazi unatakiwa kumkamilishia mwanao mahitaji yafuatayo:

(i) Daftari zenye ukubwa wa wastani au Counter book 14 au zaidi.
(ii) Kalamu za wino blue au nyeusi 2 au zaidi.
(iii) Kalamu za risasi 2
(iv) Rula, kifutio na Mathematical set 1
(v) Scientific Calculator 1
(vi) Godoro dogo la futi 21/2

(vii) Mashuka mawili rangi ya bluu bahari ( light blue )

(viii) Sanduku la chuma kwa utunzaji wa mali zake.

(ix) Truck Suit rangi ya dark blue.

(x) Vyombo vya kulia chakula.

(xi) Ndoo ndogo kwa ajili ya usafi binafsi.

(xii) Overall (ovaroli) rangi ya dark blue kwa ajili ya masomo ya Ufundi.

(xiii) Matibabu ni jukumu la mzazi hivyo wenye kadi za Bima ya afya waje nazo. Mwanafunzi ambaye hana Kadi ya Bima anaelekezwa kuja na **Tshs 50,400** ili utaratibu wa kukatuwa ufanyike.

## 4.0 MAHITAJI YA JUMLA

(i) Aje na mfagio wa chelewa mmoja (1) wenye mti kwa usafi wa mazingira ya Shule.

(ii) Aje na ufagio wa ndani 1(Soft Broom) kwa usafi wa ndani

(iii) Aje na Ream paper moja kwa ajili ya uzalishaji na ufanyikaji wa mazoezi na mitihani.

### 5.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada yakuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni( preparation);

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa ;

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na

(i) Kutunza mali za umma.

### 6.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

**(a) Wizi.**

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji.

(d) Ulevi matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharua Bendera ya Taifa.

(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.

(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kutoa mimba.

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

**(m) Kumiliki na kutumia SIMU katika mazingira ya Shule na Mabweni**

### 7.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya serikali. Fomu hii itakabidiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelekezo binafisi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***NB**: "Suala la mwanafunzi kuwa na **SIMU** halitavumiliwa na mwanafunzi akikamatwa atafukuzwa mara moja. Mzazi mueleweshe mwanao mapema".

**MAZINGIRA YA SHULE KITAALUMA NI MAZURI KWA ANAYEJITUMA KUSOMA. KARIBU SANA UPATE ELIMU BORA**

**……………………………………………………………**

**MKUU WA SHULE.**

**MWADUI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 32,**
**MWADUI – MINE. MEDICAL**
**EXAMINATION FORM**

TO: Medical Officer
______________________________________________________________________________

RE:
______________________________________________________________________________

(Name of student)
Please examine the above named Student as per Medical examination form below.

______________________

**HEADMASTER**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**
(To be completed by Government Medical Officer)
Full Name
______________________________________________________________________________

Age: ______________________________________________________________________

(I ) Blood test _____________________________________________________________

(ii) Stool Examination :_______________________________________________________

(iii) Urinary analysis __________________________________________________________

iv) STD and other V.D __________________________________________________________

(v) T.B and Leprosy test :_______________________________________________________

(vi ) Eye test:_________________________________________________________________

(vii ) Ear test: ________________________________________________________________

( viii ) Chest :_________________________________________________________________

( ix ) Abdominal test :__________________________________________________________

( x ) Speech : _________________________________________________________________

I have examined the above named student and I certify that he/she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

Signature :_____________________________________________________

Station:_______________________________________________________

Designation and Official stamp:__________________________________

Date:_________________________________________________________

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MWADUI**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi)**

1. (i) Jina la mwanafunzi ………………………………………
NB. Majina LAZIMA yawe aliyofanyia mtihani wa darasa la saba

Shule atokayo ………………………………………

(ii) Tarehe ya kuzaliwa ……………… Wilaya ……………… Mkoa ………………

(i) Dini ……………… Dhehebu ………………
(ii) Jina la mzazi/mlezi ………………………………………
(iii) Kabila ………………………………………
(iv) Namba za simu ………………………………………
(v) Kazi ya mzazi/mlezi ………………………………………

**NDUGU WENGINE KAMA WAPO**

| S/N | JINA KAMILI | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISH | NA. YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI.**

Mimi ………………………………………
ambaye ni mzazi/mlezi wa wanafunzi
……………………………………… ninakiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo yaliyotolewa kuhusu nidhamu za mwanafunzi. Naahidi kutoa ushirikiano wa kutosha katika kusimamia nidhamu ya mwanangu kwa faida ya taaluma yake.

Jina la mzazi/mlezi
………………………………………

Saini ……………… Tarehe ………………